# *Uzima Wa Milele Na Jinsi Ya Kuupokea*

. . . hapa usiku wa leo, kusikia shuhuda hizi, na matamshi mbalimbali ya shukrani kwa Mungu, kwa yale ambayo amekuwa kwao katika mwaka huu uliopita. Nami ninataka kuunganisha ushuhuda wangu pamoja nao. Nilikuwa nikiwazia, akina dada kule nyuma wakishuhudia juu ya "mkate juu ya maji." Na kisha Ndugu Slaughter. Na Ndugu Graham, wakizungumza juu ya "wakati magurudumu yote ya maisha ya kibinadamu yatakaposimama kimya." Labda tunaeleweka vibaya hapa, lakini Kule, mbele ya kile Kiti cha Enzi, Mungu anajua yote kuhusu mambo yote.

2 Kwa hivyo tuko hapa usiku wa leo kwa namna fulani . . . Siamini katika kufungua ukurasa mpya, au kitu kama hicho, mimi . . . kwamba unaurudisha tu kesho yake. Bali kama tutakuja tu na kujitolea kwa Mungu, kwa ajili ya ibada, na kumshukuru kwa yale ambayo sisi . . . Amekuwa kwetu, na kumwomba aendelee kuwa nasi, ndilo bora zaidi.

3 Nimechoka kidogo tu usiku wa leo. Nilikuwa na watu fulani jana usiku, kundi la watu, nami, vema, ni—nilikaa kwa muda mrefu kidogo. Na leo hii tulikuwa huko nje, takriban siku nzima, na kwa hivyo tunajisikia wachovu kidogo. Nami sitakaa sana hapa juu.

4 Lakini ninataka basi kumpa mimbara Ndugu Funk, naye ndiye mnenaji wetu. Na halafu Ndugu Wood, nafikiri, atamfuata. Na halafu, kwa hiyo basi, kama wote watakaa tu. Alisema, leo, nisingesema hivyo hapa. Lakini, mnaona, nilisema tu. Kwa hiyo nimemwona Ndugu Funk anayeketi kule nyuma, akitikisa kichwa chake. Huo ni mzaha kidogo kwake, ndugu. Na, lakini, hiyo—hiyo ni kweli, hakika wana majaliwa ya kufuata moja kwa moja sasa hivi, katika—katika dakika chache.

5 Na kwa hiyo tuna wanenaji wengi hapa usiku wa leo, mwajua. Kwa hiyo tuna saa tatu zilizosalia, na kwa hiyo tutajaribu tu kuharakisha upesi tuwezavyo. Wakati mwingine . . .

6 Jambo hili dogo tu ninalotaka kusema wakati huu, ni kuhusu ushuhuda wa dada pale. Dada Leopard, naamini, ndilo jina.

7 Kwa namna fulani nimefanya utaratibu mpya hapa, kama mjuavyo, majuma machache yaliyopita, ama, kuhusu watu kupiga simu ofisini. Ndipo basi—ndipo basi Ndugu Cox na hao wengine watanielezea kisa hicho, chochote kilicho. Basi

acheni niende jinsi tu ninavyojisikia kuongozwa kwenda. Na, loo, jamani, hiyo ndiyo njia ya kulifanya.

8 Hivi majuzi asubuhi, ni. . .nilikuwa nikichunguza, na simu mbalimbali. Kulikuwa na Dada Lake, na mvulana wake alipatwa na ajali. Ninaamini Ndugu Cox aliniambia ilikuwa hivyo. . .Ndugu Cox. Nao wakatoa wengu, naye ni mahututi. Ndipo ndugu mwingine ambaye nilikuwa naye tu huko milimani, mwaka huu kwenye safari, naye amelala pale, akivuja damu kwenye matumbo, labda kansa. Na huko California, loo, kila mahali tu, juu ya watu mbalimbali waliokuwa wagonjwa. Nami nilikuwa nimetoka kwenda kuomba.

9 Ndipo nikaingia, nami. . .Mke wangu alikuwa ameniambia kwamba Ndugu Slaughter alikuwa amepiga simu, jambo fulani kuhusu maskini. . .ama, Dada Slaughter, mmojawapo, kuhusu yule msichana mdogo aliyekuwa hapa Jumapili iliyopita. Niliingia tu na kuketi.

10 Nikawazia, "Vema, Mungu Mpendwa, ninao hawa wote," nami nilikuwa nikiwaombea wote. "Ba—basi unataka nifanye nini?"

Nami niliendelea kusikia kitu kuhusu "mtoto mchanga."

11 Vema, nikarudi kutazama, kuona tuliyokuwa nayo juu ya mtoto mchanga. Ndipo ni—nikampigia simu Dada Cox, ili kujua kama kuna jambo lolote kuhusu mtoto mchanga. Hakuna aliyeonekana kujua chochote kuhusu mtoto mchanga. Halikuwa ono. Bali ni kusukumwa tu katika Roho, kumtafuta mtoto mchanga, kuhusu "mtoto mchanga," mgonjwa. Vema, kitu pekee nilichoweza kupata, karibu, kilikuwa ni yule mtoto mchanga waliyekuwa wakizungumza habari zake, kutoka kule chini Kentucky. Naam, haikuonekana kama, walipotaja hilo, halikuingia vizuri, kwa namna fulani. Nami nilikuwa. . . niliwazia, pengine, labda ono lingekuja baada ya muda mfupi. Lakini halikuja, halikugeuka kuwa ono. Nami nikaendelea kushangaa.

12 Nikarudi chumbani kwangu, peke yangu, kuomba. Nami nikawazia, "Wapi, kuhusu mtoto huyo mchanga, sasa? Je, kuna mahali popote ambapo ninaweza kuwazia juu ya mtoto mchanga?"

13 Na Jumapili iliyopita, ama juma moja kabla ya Jumapili, ama kitu kama hicho, nilikuwa nimeketi kule nyuma. Ndipo msichana mdogo akaja, akaninong'onezea sikioni mwangu, nyuma yangu, akasema, "Ombea dada yangu mdogo, dada mchanga." Naye alikuwa ni yule msichana mdogo wa Leopard. Huenda akawa hapa usiku wa leo; sijui. Yeye ni jamaa mdogo sana, mwenye sura nzuri sana, msichana mdogo.

14 Ndipo ikatokea niligeuka. Nikasema, "Sawa, kipenzi," namna hiyo. Na kwa hiyo kwa namna fulani niliinamisha tu

kichwa changu na kuanza kumwombea huyo mtoto mchanga. Nami nikaendelea tu, nikasahau habari zake.

15 Na mara tu jambo hilo lilipokuja akilini mwangu, jambo fulani lilitukia, nami nikajua basi kwamba huyo alikuwa ni Mungu.

16 Hivyo basi nikaenda na kumwuliza Meda mahali—mahali walikoishi. Naye hakujua haswa, kwa hivyo tukatafuta kwenye kitabu cha simu tukapata namba yao. Na—nami nikasema, "Kitu fulani . . . Nao wana mtoto mgonjwa, naamini. Ama, juma moja lililopita, ama kitu kama hicho, juma moja ama siku kumi zilizopita, walikuwa na mtoto mgonjwa." Kwa hiyo nikasema, "Kuna jambo fulani kuhusu hilo. Sasa angalieni."

17 Nami nikapiga simu kule wala hakuna aliyejibu. Vema, basi nikampigia simu tena Bibi Cox, nami nikampata ma—mama huyu hapa, mama yake. Na—na kwa hiyo nikampigia simu mama yake, naye akasema, "Mbona . . . " Nilimwambia ilikuwa ni nini.

18 Naye huenda akawa hapa usiku wa leo. Samahani, simtambui huyo mwanamke. Ni—ningeweza kumtambua kama ningeona uso wake.

19 Lakini aliniambia kwamba huyo mtoto mchanga alikuwa hospitalini, mahututi sana, nao walikuwa wakimpa damu wakati huo. Vema, nikasema, "Dada, sijui. Siwezi kusema ni ono sasa, kwa sababu silo, bali ni kitu tu ambacho siwezi kuondoa. Kinanisukuma tu kwa—kwa mtoto huyo. Ningeweza tu, yaonekana, mtoto huyo tu mbele yangu." Kwa hiyo nikaendelea.

20 Nami nikasema, "Sitaenda sasa, kwa sababu najua itachukua muda kumwongeza damu." Nao walimwongeza kupitia kichwani hapa, nadhani, hivyo wao . . . Najua ni chungu sana na ni mbaya. Kwa hiyo nilingoja tu, nikaingia na kumwombea huyo mtoto mchanga. Nami nikajiandaa. Nikawazia, "Hapa ndipo mahali ambapo Bwana ananiongoza."

21 Nami nikakimbilia hospitalini, na—na kuomba nimwone huyo mtoto. Nao wakanipeleka pale mtoto alipokuwa. Basi humo chumbani, nikakutana na mama, ambaye yupo ameketi sasa. Naye akaniambia mama yake alikuwa amempata yapata saa moja kabla ya hapo, ama kitu kama hicho, na alikuwa amemwambia kwamba Bwana alikuwa akinisukuma, kumwendea mtoto huyo mchanga. Ndipo aliporudi kitandani; mtoto alikuwa amelala pale, akirusha mateke, akipiga makelele na kucheka.

22 Kwa hiyo nikaingia, na huyo jamaa mdogo alikuwa akirusha mateke tu na kucheka, akinyonya chupa yake ndogo, na kila kitu, wa kawaida tu kama mtoto yeyote uliyewahi kumwona maishani mwako. Nami nikaweka tu mikono yangu juu ya maskini jamaa huyo mdogo, sasa, mnaona, na kumbariki, kisha nikatoka humo jengoni.

23 Nami nikamsikia tu huyo mama akisema, dakika chache zilizopita, walikuwa tayari wamempeleka nyumbani. Basi hiyo—hiyo ilikuwa jana, wakati lilipotukia, na leo hii huyo mtoto yuko nyumbani akiwa mzima. Kwa hivyo sisi ni . . . Hiyo ilikuwa . . .

24 Hiyo ni bora kuliko mimi kupiga simu mia moja, ndani yangu. Kuwa mtulivu mbele za Bwana, apate kukwambia mahali pa kwenda hasa, na kila wakati ni kamilifu. Mnaona? Ni—ni Bwana akiongoza.

25 Sasa mtu fulani anasema, "Vema, nenda *hapa,* Ndugu Branham. Shuka *hapa* chini." U—unaingia katika machafuko makubwa sana, kwa *huyu*, *yule*, na *yule*, wewe . . . Mungu hawezi kusema nawe.

26 Kama ungeketi tu chini, useme, "Asante." Uliweke mbele za Bwana. Useme, "Sasa, Bwana, unataka nifanye nini kuhusu hili? Sasa, unajua mimi ni mtumishi Wako, na kile Wewe . . . "

27 Lakini, mnaona, Bwana akijua ya kwamba ningeenda kule mara tu Yeye aliponena na moyo wangu, alimponya huyo mtoto kabla hata sijafika kule. Hiyo ni kweli. Mnaona? Kwa hiyo, mnaona? Naam, bwana. Mnaona, haikuwa ni mimi kwenda huko.

Sasa mnasema, "Hiyo ilikuwa ni nini, Ndugu Branham?"

28 Mnaona, tuna karama katika Mwili wa Kristo. Na Roho Mtakatifu Mwenyewe, akijua hiyo ilikuwa ni nini, maombezi pale, Roho Mtakatifu alikuwa akinihimiza kwa mtoto huyo. Na mara tu nilipomwombea huyo mtoto mchanga, hata nyumbani. Ndipo nikamwendea huyo mtoto mchanga, kwa maana hiyo ilikuwa ni kutimiza yale aliyosema. Roho Mtakatifu akifanya maombezi pale, juu ya mambo ambayo hata hatuwezi kuelewa. Mnaona? Yeye si ni wa ajabu?

29 Ninawaambia, marafiki, usiku wa leo nina mengi ya kushukuru! Si—sijui jinsi ya kuanza, na hata singejaribu. Ninaninii . . . Sijui.

30 Nitasoma tu Maneno machache hapa katika Maandiko, na kuyazungumzia kwa dakika chache, Bwana akipenda.

31 Lakini, kwanza, nataka kutoa shukrani zangu kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ambaye ameniokoa na ameniosha katika Damu Yake Mwenyewe, na kunipa tumaini hili kuu na tukufu, ya kwamba siku moja nitamwona, uso kwa uso. Nami sitasimama pale katika hukumu, kwa maana Damu Yake tayari imenikomboa. Nami nimekombolewa, usiku wa leo, kwa Damu ya Bwana Yesu Kristo. Na . . .

32 Alichonipa, kuwa raia mwenzenu wa Ufalme uo huo ambao ninyi nyote mnauendea, nasi pamoja ni warithi pamoja Naye Utukufuni! Ni jambo la ajabu jinsi gani!

33 Nami nilikuwa nimeketi, jana jioni, nikizungumza na baadhi ya watu waliokuwapo wakati huo. Na leo hii, huko chini

kabisa, chini ya Elizabeth, mezani pa ndugu mmoja, ambapo tulikuwa tumeketi, tukila chakula cha jioni leo. Nasi tulikuwa tukizungumza juu ya ukweli wa kimsingi, au Injili ya msingi tuliyo nayo, na ni ukweli wa jinsi gani usio na shaka lolote. Hatuna nafasi, hata kidogo, ya shaka lolote.

34 Maskani hii, na watu, washiriki wake, na watu wa Jeffersonville na vitongoji vyake, watasimama kwenye ile Hukumu. Ikiwa hatujaokolewa, tutasimama bila udhuru wowote.

35 Siku moja, kama mhudumu kijana, wakati uamsho wangu wa kwanza ulipokuja; niliufanyia hapa pembeni, palipo na mradi huu wa nyumba, katika hema. Nilikuwa nikibatiza kundi moja kule mtoni, Jumapili hiyo alasiri, wakati Malaika wa Bwana alipojitokeza hadharani kwa mara ya kwanza, katika thibitisho la Ujumbe ambao nilipaswa kuunena. Nayo ilikuwa ni Nuru iliyoshuka kutoka Mbinguni na kusimama pale. Labda kuna watu maskanini usiku wa leo, waliosimama na kuiona Nuru hiyo. Nami nikaanza, kulisimulia, na kadhalika. Nanyi nyote mnajua hiyo hadithi inavyoendelea; na kuendelea na kuendelea.

36 Nao watu wakati mwingine wangeondoka, na kusema, “Hiyo ni dhana tu.” Wangetoka kwenye mkutano ambapo watu wangeiona, na kuondoka, waseme, “Niliiona.” Wengine wanasema, “Vema, sikuiona.”

Sasa, bila shaka, Mungu humjalia mtu kuona anayemtaka aone.

37 Wakati mamajusi walipofuata zile nyota, hakuna hata chembe moja ya historia, au chumba chochote cha uchunguzi, ama chochote kile. . . Na hata walitunza wakati kwa nyota. Lakini hakuna mtu aliyeiona Nyota hiyo ila hao mamajusi, mnaona, hiyo ni kweli, maana walikuwa wakiitafuta. Nao walikuwa wakitazamia kuiona, nayo ikawaongoza kwa Kristo. Na, hata hivyo, ilipita juu ya kila chumba cha uchunguzi, huku—huku watu wanaangalia anga, wapate kujua saa, na kadhalika. Lakini hakuna mtu aliyeiona ikienda, ila wale mamajusi, kwa maana ndio waliokusudiwa kuiona.

Kama Mungu akitaka uone kitu, utakiona.

38 Eliya huku amesimama huko Dothani, wakati ule, naye akaangalia pande zote. Naye yule mtumishi akaangalia huko nje, na kusema, “Loo, angalia. . . ” Washami walikuwa wamepiga kambi. Lakini ninii yake. . .

39 Eliya akasema, “Mbona, kuna wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao.” Akaangalia huku na huku, asingeweza kuona chochote ila Eliya amesimama pale. Akasema yeye. . .

40 "Mungu," kasema, "yafungue macho ya kijana huyu, Bwana." Na wakati, ana macho yale yale, macho ya kuona tu, hata, alipoyafungua macho yake, kote kumzunguka nabii huyo yalisimama magari ya moto na farasi wa moto. Na, mnaona, yeye . . . Ilikuwa . . .

41 Ni mahali fulani. Nasi tunajua ya kwamba Uwepo Wake upo pamoja na watoto Wake wanaoamini.

42 Nilikuwa nikizungumza, nikasema . . . Chumbani aliketi mke wangu, nasi tulikuwa tukizungumza juu ya Nuru ile ile, ambapo ilikuja na kupigwa picha.

43 Na nikirejelea tu, usiku wa leo, kwenye jambo hilo la ajabu sana, ninaamini angalau mtu mmoja au wawili, watu watatu, nadhani, walikuwako, walio jengoni sasa; ambao ni David kule nyuma, Ndugu Wood, na Dada Wood; walikuwa huko Houston, Texas, wakati ile picha, Mungu alipoiruhusu ipigwe.

44 Sasa, kama ulisimama usiku wa leo, na kumtazama Malaika huyo, akizunguka! Kuna wengi wenu hapa ndani, labda, hamjawahi kumwona. Lakini, mnaona, hiyo Nuru, Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli! Hiyo ilikuja kwenye vyumba vidogo vya gereza pamoja na Petro, na—na—na kumtoa gerezani; Malaika yuyu huyu wa Bwana. Naye Huyu hapa, baada ya mamia hayo yote, naam, maelfu ya miaka, angali hapa pamoja nasi sasa. Mnaona? Naye amepigwa picha Yake, akisimama mahali nilipokuwa nimesimama. Sasa, hapana, si kwa ajili yangu; bali kwa ajili ya Kanisa, kwa ajili ya Mwili wa waaminio. Mnaona, ni kwa ajili ya kila mtu. Sasa angalieni. Kama . . .

45 Ni—ninaamini ya kwamba kweli ilikuwa ni Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli. Hivi hamwamini hivyo? Nguzo tu ya Moto.

46 Nami kwa kweli ninaamini ya kwamba Nuru hiyo ilikuja gerezani, na—na—na ambapo Petro alikuwa. Je, hamwamini ushuhuda huo? Ninaamini kwa moyo wangu wote, zaidi tu ya vile ninavyoamini jina langu ni William Branham. Ni—ninaamini hiyo, mnaona. Ninaiamini hadithi hiyo.

47 Lakini, hata hivyo, tuna thibitisho lake lililo la kimsingi na thabiti zaidi, kuliko hilo. Tunalo. Tunalo thibitisho la kimsingi lililo thabiti zaidi. Sasa, ninaamini hilo kwa imani.

48 Na vipi kama huyo Malaika wa Bwana angekuwa amesimama hapa sasa, akizunguka, na kila moja la macho yenu lingeweza kumwona. Hilo lingekuwa ni jambo zuri sana. Lakini kuiangalia picha Yake, ni thibitisho kubwa zaidi kuliko vile ungeitazama kwa macho yako. Unaona? Sivyo? Kwa sababu, unaweza kushikwa na udanganyifu wa macho. Lakini huo mta- . . . Kamera hiyo haitapiga picha udanganyifu wa macho. Haitafanya hivyo, kwa sababu ni—ni kamera. Nayo

itapiga picha halisi. Haina budi kuweko, ipate kuigusa hiyo lenzi. Mnaona?

49 Unaweza kuwa na udanganyifu wa macho, na vitu vinavyoonekana kana kwamba ndivyo, wakati sivyo. Mnaona? Lakini wakati picha hiyo . . .

50 Na inaweza kuwa saikolojia. Unaweza kusema, "Unaiona ile pale?" Na uendelee tu kusema, "Naam, ninaiamini." Na uamini sana mpaka kwa kweli unafikiri unaiona, wakati huioni. Unaona? Hiyo ni kweli. Lakini, hiyo ni saikolojia. Lakini, wewe, ilikufanya ushinikizwe sana kiakili kuielekea, mpaka u—unaiwazia tu, unaiwazia sana hata inakuwa halisi.

51 Unafikiria tu mtu anakuchukia, mara moja. Wala hawakuchukii, lakini unawazia wanakuchukia. Nawe unaendelea tu kuwazia, "Hawanipendi." Ndipo muda si muda, utakuwa ukimkwepa mtu huyo, wakati hajakufanyia lolote. Na baada ya muda, inakuwa halisi sana kwako, mpaka unaamini kwa hakika kwamba mtu huyo hakupendi. Na huenda ukawafokea, au kusema jambo fulani kwako. Kwa mfano, mke wako, au mume wako, au jirani fulani, ama kitu kama hicho, wakati, mtu huyo kabisa hana hatia ya ubaya wowote. Ni kwa sababu unaiwazia tu hivyo, lakini, mpaka itakapokuwa halisi kwako. Sasa mnaona ninachomaanisha?

52 Lakini, kwa kweli, wakati picha inapopigwa, lazima iwepo.

53 Kwa hiyo, usiku wa leo, tumepitia, kama vile Ndugu Graham alivyoeleza muda mfupi uliopita, heka heka nyingi za kanisa, na kadhalika. Tumepitia hatari nyingi, taabu na mitego; ambayo imewaziwa tofauti, walisema tulikuwa "wasiojali," na "watakatifu wanaojifingirisha," na majina ya kila namna, na kadhalika, namna hiyo.

54 Lakini, hata hivyo, katikati ya hayo yote, kama maskani hii ingeteketezwa, usiku wa leo, nami nife, nanyi wengine muondoke, pia, usiku wa leo, ushuhuda wetu ni wa Kweli kabisa. Kuna mamilioni ya watu ambao wamejua habari Zake. Nalo thibitisho la kisayansi linathibitisha; si neno letu tu, yale tuliyosema kabla ya ile Nuru, kabla Malaika hajapata kupigwa picha Yake. Ilishuhudiwa, tangu utotoni, ya kwamba Nuru hiyo ilikuja. Miaka mingi, wengi wenu mnaoketi hapa, mlinisikia nikizungumza juu yake, miaka na miaka, na kujua yote kuihusu, miaka na miaka kabla hiyo picha haijapigwa. Ndipo wakati ulimwengu wa kisayansi ulipopata picha Yake, ilikuwa ni kitu kile kile kabisa tulichoshuhudia. Kwa hiyo hiyo inaonyesha unasema Kweli. Ni Kweli kabisa.

55 Kwa hiyo, usiku wa leo, ninashukuru sana kujua kwamba Yehova Mungu mkuu, ambaye wakati mmoja alinguruma kutoka Mlima Sinai, ambaye wakati mmoja alisimama juu ya mlima na kufundisha zile heri, kisha akafufuka katika wafu, yuko katikati

yetu usiku wa leo, na ni yeye yule. Kama alivyokuwa wakati huo, ndivyo alivyo leo, na atakuwa milele.

56 Na kuwazia ya kwamba Yeye, Mungu wa Mbinguni, angejiaibisha Mwenyewe, kushuka na kushirikiana na watu kama mimi na sisi hapa, watu maskini, wasio na mengi ya ulimwengu huu. Na wasio na elimu, kama nilivyo mimi, na hata hivyo alinipenda sana, hata akashuka na kuniokoa kwa neema Yake. Hakuna nilichostahili, au, nisingeweza kufanya, bali Yeye aliniokoa. Kwa sababu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alinichagua tangu zamani nipate kuokolewa, katika kujua Kwake tangu zamani, kabla ulimwengu haujaanza. Na kila mtu mwingine aliyeokolewa, Yeye aliwafanyia jambo lile lile. Loo, ni jambo la ajabu jinsi gani! Ni fursa nzuri jinsi gani!

57 Na shauku ya moyo wangu wote ni, kwa mwaka huu, ikiwa Mungu atasikia maombi yangu . . .

58 Huenda nisiweze kukaa sasa hadi usiku wa manane kamili. Nina wasichana wawili wadogo kule nyuma, ambao hushikwa na usingizi, nao wanaanza kunung'unika na kulia. Huenda ikanibidi kuwapeleka nje, kwanza.

59 Nami ninataka kusema hivi, kama sitapata nafasi ya kurudi huku na kushuhudia, kwamba ni—nina . . . nataka kumshukuru kila mmoja wenu kwa ajili ya maombi yenu ambayo mmeniombea mwaka huu. Kama mkiniachilia, nimekwisha. Ni vile tu mnavyonishikilia, katika maombi, hivyo ndivyo ninavyoenda vitani.

60 Na mimi—mimi nawapenda, kama ndugu mmoja alivyosema muda mfupi uliopita, kwa moyo wangu wote. Sipati kuja hapa kama inipasavyo. Sipati kuwaona watu na kuwahudumia nyumbani, kama ni—nitakavyo, kama moyo wangu ulivyo. Lakini mimi ni mwanadamu tu, na ni—nina kikomo cha saa fulani na nguvu kiasi fulani, na kadhalika.

61 Na sasa, lakini kwa msaada wa Mungu, kama atanisaidia, nataka mwaka huu uwe mwaka mkuu zaidi ambao nimewahi kuwa nao maishani mwangu. Sasa, kwa neema ya Mungu, nimewaleta zaidi ya watu nusu milioni kwa Kristo. Nami natumaini, mwaka huu, kufikisha milioni kamili, Mungu akipenda. Maana, Mungu akipenda, ninataka kuanza kupitia n—nchi za kigeni tena, mara tu tunapokuwa na uwezo kifedha, na kadhalika, kufanya hivyo. Na kuingia katika nchi zingine huko, ambako tunaleta maelfu kadhaa kwa wakati mmoja.

62 Nami najua kwamba siku imekaribia. Saa zimeenda sana. Utusitusi unaingia, enyi marafiki. Nami ninataka kufanya yote niwezayo, kwa maana huu ndio wakati pekee ambapo mimi na wewe tutawahi kuwa wanadamu. Huu ndio wakati pekee ambao tutawahi kuwa na fursa, katika Umilele wote, kumleta mtu kwa Kristo. Na tufanye hivyo. Kila kitu tunachoweza kufanya. Hebu na tuweke kila saa, tuwezayo, kwa Utukufu Wake. Hiyo ndiyo

nia yangu kwa mwaka huu ujao. Na kwa msaada wa Mungu, maombi yenu, nitafanikiwa. Kwa hiyo, niombeeni sasa.

63 Na sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, kwa ajili ya kufunguliwa kwa Neno.

64 Baba, hili ni Neno Lako la Milele lililo hapa mbele yangu. "Hakuna mtu Mbinguni wala duniani aliyestahili kukitwaa kile Kitabu, kuifungua ile Mihuri, ama kuitazama, ila Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Sasa tunamwita Yeye. Na kama tumepata neema machoni Pako, tunaomba, Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, ya kwamba utachukua dakika hizi chache sasa, tunapofungua kurasa za Neno Lako, na kulifungua kwa mioyo yetu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

65 Sasa, nilikuwa nikitaka kusoma, muda kidogo tu alasiri ya leo, juu ya mambo machache ya kuzungumzia, kwa ajili ya usiku wa leo, lakini sikuingia kwa wakati mzuri kufanya hivyo. Kwa hiyo mke wangu akashuka pamoja na Billy, ndipo i—ikanibidi kuitwaa tu na ku—kuigusagusa tu Biblia.

66 Nami nikawazia, "Vema, nitapitia hilo, Melkisedeki." Kisha nikawazia, "Loo, jamani! Kama nikiliendea hilo, hao wengine, ndugu, hawangekuwa na wakati wa kuzungumza." Na kwa hiyo, juu ya hilo, ninalishikilia hilo katika siku chache, Bwana akipenda, wakati tukiwa na muda mwingi, sasa.

67 Ndipo nikapata mlango wa 10 wa Matendo, ukinena juu ya Kanisa la mwanzoni. Kama mtu yeyote akitaka, na anayo Biblia, ambaye angefungua Matendo mlango wa 10, kwa mawaidha kidogo tu kwa dakika chache.

68 Na wakati mkifungua, nitatoa mapitio kidogo ya awali. Jumapili iliyopita, juma moja lililopita, naamini sasa, ama ilikuwa ni Jumapili iliyopita, juma moja lililopita, ambapo tulisoma katika Kitabu cha Matendo, kuhusu Kanisa la mwanzoni. Tulikuwa katika Matendo 2, naamini. Ambapo walipoachiliwa, na wakaenda zao... Jinsi ilivyo... Petro akawaambia, jinsi ilivyowapasa "kutubu, na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Roho Mtakatifu."

69 Sasa ningependa kutoa tamshi dogo. Je, lolote li sawa, usiku wa leo, kutoka jukwaani? [Ndugu Neville anasema, "Amina."—Mh.]

70 Angalieni, tazameni, kila mtu sikuzote amesema, "Ndugu Bill, hakuna mtu anayekuelewa." Vema, labda mimi ni wa ajabu ajabu kidogo, lakini, mnajua, lakini si—sikusudii kuwa hivyo. Lakini nina mawazo ya mambo, na imani yangu. Sasa, nimeninii kabisa...

71 Nimeshawishika kabisa ya kwamba mambo mengi, yaliyo—yaliyo kwenye Maandiko, ambayo ni ya kimitume, ambayo hatuyatekelezi, siku hizi.

72 Na, kwa mfano, jambo moja, watu wengi wamesema, "Jinsi, unapokuwa huko nje katika mikutano hiyo ya uinjilisti, unawezaje kuwaleta watu elfu thelathini madhabahuni waokoke?" Si lazima waje madhabahuni kuokoka. Jambo pekee wanalopaswa kufanya ni kumwamini Bwana Yesu Kristo. Hiyo ni kweli?

73 Ninataka tu kuwaulizeni jambo fulani, nanyi mliwazie, kisha nitapokea barua zenu juma hili lijalo. Mnaona? Je . . .

74 Siwezi kuwa Mkatoliki. Lakini, Katoliki inaamini Neno hili limevuviwa, lakini, "Kanisa liko juu ya Neno." Siwezi kuwa Mprotestanti. Kwa maana, Waprotestanti huchukua tu kiasi wanachofikiria ni sawa, na, "Mengine hayajavuviwa."

75 Kwa hiyo, ninaamini yale Biblia isemayo, kwamba ni Kweli. Ninaamini ya kwamba Hilo ni Neno la Mungu. Ili kuamini Hilo, sina budi kusalimisha maisha yangu yote na nia yangu yote kwa Hilo, kuamini ya kwamba Hilo ni la Kweli, ya kwamba hakuna Kweli nyingine ila Hiyo. Hakuna cha zaidi cha kuongezwa Kwake, wala hakuna cha kuondolewa Kwake. Hivyo ndivyo tu linavyopaswa kuwa. "Na mtu yeyote atakayeondoa katika Kitabu hicho, ama kuongeza Kwake, huyo ataondolewa katika Kitabu cha Uzima," alisema Mungu, katika Ufunuo. "Kila atakayeondoa, au kuongeza katika Hili!" Hayo ni mapenzi makamilifu ya Mungu, na ufunuo wa Yesu Kristo, kwa watu. Hiyo ni kweli. Sasa, ili kufanya hivyo, sina budi kuamini ya kwamba Neno la Mungu ni Kweli kabisa.

76 Na katika Matendo 2:38, Petro aliposema, "Tubuni, kila mmoja wenu!"

77 Walisema, "Wanaume na ndugu zetu, tufanye nini?" kwanza. Walitaka kuokolewa.

78 Sasa angalieni. Anazungumza pale na wasioamini. Sasa angalieni alichosema. Alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu!" Sasa *kutubu* maana yake nini? *Kutubu* maana yake ni "kujutia yale uliyofanya."

79 Kwa mfano, vipi kama ningegeuka papa hapa sasa na kumpiga ndugu yangu, bila sababu. Nami ninataka kulitubia; ningesema, "Ndugu Neville, samahani nilifanya hivyo." Mnaona? Naam, basi, nikisema, "Samahani nilifanya hivyo," na kulimaanisha kutoka moyoni mwangu, nimetubu.

80 Na ikiwa nimezijutia dhambi zangu, na kumwomba Mungu anisamehe, nimetubu. Hiyo ni kweli? Sawa. Petro alisema, "Tubuni, au mzijutie dhambi zenu, kisha mbatizwe kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea

kipawa cha Roho Mtakatifu." Hiyo ni kweli? Vema. Nyumbani, wakati . . .

81 Paulo na Sila walikuwa wamefanya mkutano, na walikuwa wamewekwa gerezani, wakapigwa, kwa sababu walimtoa pepo mchafu kutoka kwa yule mpiga ramli. Na walipokuwa katika gereza la Filipi. Basi usiku huo, walipoimba nyimbo, nao . . . Bwana akatuma tetemeko la ardhi, na kutikisa gereza kwa nguvu sana hata, pingu, zikaanguka kutoka kwenye mikono yao. Mlinzi wa gereza akachomoa upanga wake, ili ajiue. Naye Paulo akasema, "Angalia usijidhuru, kwa maana sote tuko hapa." Naye akasema . . . Afanye nini apate kuokolewa? Akasema, "Mwamini Bwana Yesu Kristo, pamoja na nyumba yako yote . . . moyo wako wote, nawe utaokolewa, wewe na nyumba yako." Angalieni, "Mwamini Bwana Yesu Kristo."

82 Sasa, ikiwa mtu amezijutia dhambi zake! Ninataka tu kuichukua kwa urahisi, ili izame kwenye kilindi. Kama mtu amezijutia dhambi zake, na atubu, kwa kuwa anazijutia dhambi zake, na kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wake, kutoka kwa dhambi zake, na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo; Mungu anawajibika, dakika iyo hiyo, kumpa huyo mtu ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kama sivyo, hawezi . . . Yeye hakulitimiza Neno Lake. Hiyo ni kweli?

83 Sasa, mbona mikutano yote ya kungojea, basi? Mbona ushahidi wote na kadhalika tunaopaswa kuwa nao?

84 Sasa, Yesu alisema, Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye alisikiaye neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele." Sasa, kama "Uzima wa milele," neno *milele* linamaanisha nini? Hilo linamaanisha, "bila mwisho." Kama yeye—kama yeye . . . "Yeye asikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima usio na mwisho."

85 Mbona huko kurudi kwote na—na kujaribu kuokolewa tena, na mambo haya yote, basi?

86 Kama una Uzima usio na mwisho, huwezi kuangamia. Maisha yako hayawezi, kwa sababu unao Uzima wa Milele.

87 Sasa, kama baadhi yenu wangetaka kulichunguza neno hilo, mtapata mle ndani, neno la Kiyunani, lina *Zoe*, Z-o-e, neno la Kiyunani, ambalo linamaanisha "Uzima wa Mungu."

88 Kwa sababu, kama ni wa milele, kuna kitu kimoja tu ambacho ni cha milele, nacho ni Mungu. Yeye ni, "Tangu milele hata milele, Wewe ni Mungu." Sasa, ikiwa Yeye ni kutoka milele na hata milele, na amekupa milele hata Uzima wa milele, basi itabidi uwe sehemu ya Utu Wake wa milele. Je, hiyo ni kweli? Na ukifanyika sehemu ya Utu wake wa milele, hiyo inakufanya kuwa mwana au binti Kwake; ambalo linatimiza kabisa yale ambayo Maandiko yanasema, "Sisi ni wana na binti za Mungu." Je, hiyo ni kweli?

89 Ulimpata lini? Wakati ulipopaza sauti? Ulipoenda madhabahuni? Uliponena kwa lugha? Ulipoamini! Tunawabatiza wengi sana ambao hawaamini. Tunawasikia wengi sana, wakinena kwa lugha, ambao hawaamini. Tumewachochea kwa ushahidi, na kufanya mambo, na kuwapangia, tukisema, "Unapofanya *hivi*, umempata." Hakuna kitu katika Biblia, hakuna mahali popote katika Biblia, ambapo unaweza kumhakikishia mtu, "Kwa sababu anafanya *hivi*, kwamba yeye ni Mkristo."

90 Yeye ni Mkristo kwa sababu anaamini. Nayo maisha yake mwenyewe huzaa tunda la Roho, haijalishi anafanya nini. Mnaona? Ndivyo ilivyo. Sasa, na unapoamini, unapokea Uzima wa milele. Nao Uzima wa milele ni Mungu; naye Mungu ni Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli?

91 Ikiwa Mungu na Roho Mtakatifu si Mtu yule yule, Yesu alikuwa na Baba wawili. Yesu alisema kwamba "Mungu" alikuwa Baba Yake, nayo Biblia inasema kwamba "Roho Mtakatifu" alikuwa ndiye Baba Yake, kwa hiyo wote wawili walikuwa Mtu mmoja.

92 Na kama ukimpokea Mungu, Uzima wa Milele ndani yako, basi umepokea nini? Hilo ndilo ninalotaka kujua. Mnalipata hilo wazo?

93 Tumejawa sana na nadharia, kanisa limejazwa, kwa sababu limeundiwa dhehebu. Dhehebu hili linapata *hili*, wanaamini *hili*, wanaunda madhehebu kutokana nalo. Hawawezi kusonga mbele zaidi ya hapo.

94 Lakini Kanisa la Mungu daima linasonga mbele, likiendelea. Linasogea moja kwa moja na kuyaacha madhehebu yameketi nyuma. Liliondoka kwa Luther. Liliondoka kwa Methodisti. Liliondoka kwa Baptisti. Liliondoka kwa Presbiteri. Na linaondoka kwa Pentekoste. Hakika. Maana, Uzima wa milele unaendelea mbele, mnaona, nawe unaupata kwa sababu (kwa nini?) unamwamini Bwana Yesu Kristo.

95 Sasa kuna mambo mawili tu. Angalieni. Ama wewe ni asiyeamini au mwaminio.

96 Ama ni mchana au ni usiku. Hiyo ni kweli? Sasa, siwezi kusema, "kiasi *hiki* tu cha huu ni—ni—ni usiku. Ni kile tu ninachokiona kupitia kwenye dirisha hilo, hicho ndicho usiku." La, la. Kitu hicho chote ni usiku. Hiyo ni kweli.

97 Sasa, kuvu-. . .kama ninavyosema mara nyingi. Kuvuta sigara, kutafuna tumbaku, na kunywa wiski, hiyo siyo dhambi. Hayo ni matokeo ya dhambi. Unafanya hivyo kwa sababu wewe ni asiyeamini.

98 Na kuishi kwa haki, na utakatifu, na amani, na shwari, na utulivu, na kupendeza, na—na kirafiki, na kadhalika, hiyo si kwa sababu wewe ni Mkristo. Hizo ni sifa tu za Ukristo.

Ni kwa sababu ya kile kilicho ndani yako, hufanya hivyo. Na kama unaliigiza, ama unalifanya kwa sababu unadhaniwa kuwa Mkristo, wewe ni mnafiki, hiyo ni kweli, ikiwa maisha yako hayaishiwi kwa utamu. Kwa sababu, ndani yako, Kitu fulani kinatokea. Kinafanya hivyo, kinakufanya ujisikie hivyo.

99 Utapitia majaribu, na shida, na kupanda na kushuka, na kueleweka vibaya. Hilo halina uhusiano wowote Nalo.

100 Wakati Israeli waliporudi nyuma na kushuka kwenda Misri, walikuwa wamerudi nyuma. Hawakupoteza agano lao kamwe. Walipoteza furaha ya wokovu wao.

101 Daudi hakusema, "Unirudishie wokovu wangu." Alisema, "Unirudishie furaha ya wokovu wangu." Ilibidi wokovu wake ubakie vile vile. Lakini alienda kombo na kupoteza furaha ya wokovu wake. Mnaona ninalomaanisha?

102 Uliokoka lini? Ulitakaswa lini? Ulijazwa lini na Roho Mtakatifu? Ulipomwamini Bwana Yesu Kristo! Kwa maana, ulipokea, hapo, Uzima wa milele.

103 Lakini basi, tangu wakati huo na kuendelea, ulianza kukua. Ulianza kukua. Ulikua kupitia utakaso, kupitia Roho Mtakatifu, na kupitia kunena kwa lugha, na kupitia mambo haya yote hapa.

104 Lakini ulipokea Uzima ulipoamini. Unaona ninachomaanisha? Na sasa hilo halininii. . .Baadhi ya watu tayari wana Uzima, nawe unajaribu kuwafanya wafanye jambo fulani *hapa,* wakati hawajafika mahali hapo bado. Nao Wapentekoste hawajawahi. . .wamefikia mahali ambapo Kanisa linafikia sasa, kwenye kufanywa wana wenye mamlaka, au kuwekwa wana mahali pao.

105 Sasa, katika Agano la Kale, wakati mwana alipozaliwa katika nyumba, alikuwa ni mwana kwa sababu alizaliwa nyumbani. Mwanangu ni mwanangu alipozaliwa kwangu.

106 Na wakati Kanisa la kipentekoste lilipojifungua, ama walipopata kile walichoita "Kuzaliwa, Kuzaliwa upya, au Kanisa la Roho Mtakatifu," kwamba walizaliwa katika Ufalme wa Mungu.

Vema, sasa, katika Agano la Kale. . .

107 Sasa, katika Waefeso, mlango wa kwanza, lilisema, "Tumechaguliwa tangu zamani tufanywe wana." "Kwa kufanywa wana wenye mamlaka"? Angalieni hilo, "Kufanywa wana wenye mamlaka!" Naam, bwana.

108 Na mtu, katika Agano la Kale, alipozaliwa mwana nyumbani mwake, alikuwa ni mwana alipozaliwa. Lakini kulikuwako na mwalimu aliyemlea mtoto huyo mpaka akafikia umri fulani. Ndipo kama mwalimu huyu alikuwa. . .alileta habari kwa baba, ya kwamba mtoto huyo alikuwa anastahili na yuko sawa, na kadhalika, sasa, ilibidi. . .Basi—basi alifanywa mwana mwenye mamlaka katika familia hiyo. Wengi wenu ninyi wasomaji

wa Agano la Kale mnajua Maandiko juu ya hilo. Alifanywa mwana mwenye mamlaka katika hiyo familia. Lakini kama hakufanywa, bado alibaki kuwa mwana, ila hakufanywa mwana mwenye mamlaka. Na basi kama alifanywa mwana mwenye mamlaka, alitolewa nje mtaani, akavikwa joho, halafu sherehe ikafanywa. Ndipo basi sahihi ya mvulana huyu, kwenye hundi, ilikuwa sawa tu na ya baba yake. Sawa kabisa, kwa kuwa alifanywa mwana mwenye mamlaka katika ushirika kamili wa familia.

109 Mungu alimfanya Mwanawe Mwenyewe mwana mwenye mamlaka, hapo alipompandisha juu; akawachukua Petro, Yakobo na Yohana, kama shahidi. "Kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno na lithibitishwe." Kisha akapanda huko juu, naye Mungu akamtia Kristo uvuli. Roho Mtakatifu alimtia Kristo uvuli, nayo mavazi Yake yakang'aa kama jua. Hiyo ni kweli? Naye Mungu Mwenyewe akasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa. Msikieni Yeye." Kwa maneno mengine, "Huyo hapo. Anachosema kinatosha." Na kisha akapewa ninii sawa...Na, bila shaka, ilikuwa ni Mungu, bali Mungu katika mwili wa Yesu Kristo, akijidhihirisha Mwenyewe kwa watu. Na, hapo, Mungu alimfanya Mwanawe Mwenyewe mwana mwenye mamlaka.

110 Na sasa wakati kanisa la Kipentekoste na watu hawa katika siku za mwisho hapa walipoanza kushika Kuzaliwa upya, kuzaliwa mara ya pili, walifikiri hilo lilitosha. La, bwana. Mahangaiko yenu, na shida zenu, na mambo kama hayo, Mungu hawezi kukuweka kama mwana.

111 Lakini unapokaa katika Ufalme, unapokaa katika Injili, unapokaa sawa, moja ya siku hizi Mungu atakuita na kukuweka kando, na kukufanya kuwa mwanawe mwenye mamlaka, mbele ya watu, na kukupa kitu ambacho utayatikisa mataifa, nacho. Unaona ninachomaanisha? Ni kufanywa mwana mwenye mamlaka katika familia.

112 Sasa, hawa waliokuwa wamemfuata; Petro, Yakobo, na Yohana. Tunazungumza usiku wa leo juu ya Petro, ono kuu, jinsi watu hao walivyoishi katika siku hiyo.

113 Na sasa, kwanza, hapa kwenye ishirini na-...au, kifungu cha 32 cha mlango uliotangulia, m—mlango wa 9.

> *Hata Petro alipokuwa akizunguka pande* zote,... *akawatelemkia*...*watakatifu* waliokaa Listra.
>
> *Akamwona mtu mmoja huko jina lake Ainea, amelala*...*mtu huyo amelala ki—kitandani mwake miaka minane, maana alikuwa amepooza.*
>
> *Petro akamwambia, Ainea, Yesu Kristo akuponya: ondoka, ujitandikie. Mara akaondoka.*

114 Litazame. Sasa angalia kilichotokea.

> *Na wote waliokaa Lida na Sharoni*. . .(Angalieni hapa.). . .wote *wakamgeukia Bwana*.

115 Kwa sababu mtu aliyepooza aliponywa, nchi nzima ikamgeukia Bwana, kwa kuwa mtu mmoja alikuwa ameponywa, aliyekuwa amepooza.

116 Na, siku hizi, wafu wanafufuliwa. Nao watu wanasema, "Ni elimu ya pepo. Ni saikolojia. Ni telepathia ya kiakili. Huyo mtu hakuwa amekufa, kwanza kabisa." Mnaona tofauti yake? Ni kutokujali kwetu kwa Mungu, kumeamua kile tunachopata leo. Tutapokea hukumu ya Kiungu. Ulimwengu mzima unatetemeka hivi sasa, chini ya athari za hukumu zinazonyemelea.

117 Mmoja wa wahudumu labda atalichukua, katika dakika chache, juu ya hukumu zinazokuja. Nami natumaini watafanya hivyo, kwa vyovyote vile, kwenye, hukumu ijayo.

118 Kwa sababu, ulimwengu mzima uko tayari, unatetemeka. Kila taifa linatetemeka. Msifikiri kwamba Urusi haitetemeki, pia. Marekani na visiwani inatetemeka. "Ni nani atakayerusha hilo bomu la kwanza la atomiki?" Itakapotukia, huenda ikakivuruga kitu hicho chote, wala pasiwe na. . .ambaye. . . Bomu la kobalti, vipi kama machache yake yataachiliwa? Hakutakuwako na hata nzi au mdudu juu ya uso wa dunia atakayesalia.

119 Sasa iko mikononi mwa watu waovu, wenye dhambi, wanaoelekea kuzimu. Na kikomo chako cha safari ya dunia hii, nilisema, safari ya dunia, kimeachwa mikononi mwa watu waovu na wenye dhambi. Afadhali uangalie mahali ambapo kikomo cha nafsi yako kimeahidiwa. Ikiwa hakijaahidiwa Mbinguni na kwa Mungu, geuka usiku wa leo, kwa moyo wako wote, wala usiache huu mwaka unaoisha kupita bila wewe kumgeukia Mungu. Kwa maana, kikomo chako cha duniani kimeamriwa na mikono ya watu waovu, na katili, wasio na huruma, makafiri. Huko ndiko mwili wa—wako umeamriwa. Lolote wanalotaka kuufanyia sasa, hilo linakumaliza. Mungu aturehemu!

120 Naye Mungu, katika rehema Zake za upendo, akituma ishara, na maajabu, na miujiza, na kadhalika, na kuihubiri Injili, huku watu wakielekeza uso wako siku zote kwenye. . .mbali Nalo. Basi unawezaje kutarajia kitu kingine isipokuwa hukumu? Lazima uipokee.

121 Na mtu mmoja akiwa ameponywa kupooza, na nchi nzima ikamgeukia Kristo!

122 Na hapa ambapo tunao wafalme, na wenye mamlaka, watawala, na wabunge, na kila kitu kingine; mateso, na magonjwa, nao wamekufa na kuaga dunia, na kuwaona wakifufuka wapate kuishi tena, nalo taifa linalidharau tu na kulicheka. Basi tumebakiwa na nini ila hukumu?

123 Loo, ndugu, kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo Mungu aliwaamsha watu Wake, ni leo. Mwaka huu ujao, Mungu na awatie mafuta wahudumu Wake, kama miali ya moto, kwa maana mko katika siku za mwisho, na nyakati za kufunga.

124 Angalieni hapa. Mtu yuyu huyu alishuka. . . Kulikuwa na msichana mmoja jina lake Tabitha, linalomaanisha "Dorka," aliyekufa alipokuwa huko chini. Naye Petro alikuwa huko Yafa. Wakatuma mtu wakamwita, wakamleta huko chini. Naye akaingia mahali alipokuwa amelala, maiti. Akawatoa watu wote nje, akapiga magoti na kuomba. Naye alipofanya hivyo, akaenda huko na kumshika mkono, na kumwinua. Naye akawa mzima tena, hai.

125 Basi angalieni kilichotukia. "Ikawa, alikaa siku kadha wa kadha." Kabla tu ya hapo:

> *Ikajulikana katika mji mzima wa Yafa; wengi wakamwamini Bwana.* Wengi wakaamini!

126 Na, leo hii, wangesema, "Nina shaka kama alikuwa amekufa kabisa, ama la. Alikuwa tu a—amezimia ama kitu kama hicho. Siamini kitu kama hicho." Walielezee vinginevyo kabisa! Unapoelezea mambo ya kimbinguni vinginevyo, kutoka katika Biblia, unamwelezea vinginevyo Mungu yule yule unayemwabudu. Bila shaka, ndivyo unavyofanya. Yeye ni Mungu wa kimbinguni. Vema.

127 Sasa, lakini, ati uwakomeshe mitume hawa? Ndugu, walikuwa pamoja na Yesu. Hawakujali mtu yeyote alisema nini. Waliwaita kule wakati mmoja na kuwaambia ya kwamba siku za miujiza zilikuwa zimepita. Na kuwapiga mijeledi na kuwatia gerezani, na kuwaweka usiku kucha, na kesho yake asubuhi wakawaleta hukumuni. Ndipo, wakaja kugundua, walikuwa watu wasio na elimu wala maarifa. Lakini wakatambua, kwamba walikuwa pamoja na Yesu.

128 Walipoachiliwa, hawakwenda kule na kushauriana na seminari tena. Walienda kwa watu wao wenyewe. Nao walipokusanyika, wakieleza aliyoyafanya Bwana, walikusanyika pamoja na kuomba maombi haya, "Bwana, kwa nini. . . " Ni kutimiza yale yaliyonenwa na nabii, bila shaka, "Mbona makafiri wamefanya ghasia, na makabila wakatafakari ubatili?" Kasema, "Kweli utupe nguvu, kwa kuunyosha mkono wa Mtoto Wako Mtakatifu Yesu, kuponya wagonjwa, na ishara na maajabu yapate kufanywa." Basi watu hao walipoomba kwa moyo mmoja mahali hapo, hilo jengo lilitikiswa, ambamo walikuwa wamekusanyika pamoja.

129 Tunachohitaji usiku wa leo ni umoja, mkutano wa maombi, ambapo tunajifunga pamoja kwa moyo mmoja na nia moja, na kuomba maombi kama hayo, ndipo tutakuwa na wakati mwingine wa kutikiswa. Amina.

130 Angalieni. Petro, aliyekuwa mkana Bwana wakati mmoja, wakati mmoja hakumwamini, au alikuwa amemkana; kisha akatoka nje na kulia kwa uchungu, halafu akaingia ndani. Sasa amempokea Roho Mtakatifu. Msikilizeni akihubiri.

> *Basi palikuwa na mtu* jina lake…au, *aitwaye Kornelio, akida wa kikosi kilichoitwa kikosi cha Kiitalia,*
>
> *Mtu mtauwa,…mtu aliyemcha Mungu, yeye na nyumba yake yote,* naye *aliwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu* sikuzote.

131 Ni mtu wa jinsi gani! Sasa, sio, kumbukeni, sio…Hata Mmataifa. Hata si Myahudi. Alikuwa Mmataifa, akida; mkuu wa mia moja, ni watu mia moja. Lakini alikuwa mtu anayemcha Mungu. Mungu daima, miongoni mwa watu wa Mataifa, amepata watu wanaomcha Mungu.

132 Wakati nikitembea leo na kuzungumza na kijana mwanamume mmoja, nilisema, "Nitakapofika Mbinguni, moja ya mambo ninayotaka kufanya ilikuwa ni kupanda juu na kupeana mikono na jamaa fulani ambaye alikuwa amefanya jambo la kishujaa." Naye akazungumza juu ya yule ambaye yeye alitaka kumwona. Alitaka kumsalimia kwa mkono, kuhusu mambo mbalimbali, jinsi ambavyo Mungu aliwabariki watu.

133 Wakati, Uria, baada ya Daudi kumtwaa Bathsheba, mkewe, nao wakatuma watu wakamleta. Naye alikuwa mja mzito. Naye akamwingiza ndani, ili apate kumwekelea Uria. Naye hakuwa Mmataifa…Hakuwa Myahudi. Alikuwa Mmataifa, naye alikuwa Mhiti, mwongofu wa dini ya Kiyahudi. Naye akamwambia ashuke aende na kukaa kwa muda nyumbani, pamoja na mke wake mrembo, mzuri. Akasema, "Mungu aniepushe nisifanye jambo kama hilo, na sanduku la Mungu wangu liko kwenye uwanja wa vita." Naye akakataa kufanya hivyo.

134 Na, ndugu, nitakapofika Utukufuni, ninataka kumwendea Uria na kumpa mkono, na kusema, "Mungu asifiwe, kwani ushuhuda wako ulimaanisha kitu kwangu katika safari yangu ya duniani."

135 Ninataka kumwendea Danieli, niseme, "Unajua, Danieli, ulipoingia mle bila woga mbele ya hao simba, ushuhuda huo ulimaanisha kitu kwangu." Naam, bwana.

136 Nataka kumwona mtume, Petro, na kusema, "Petro, usiku ule ulipokuwa gerezani, naye Bwana akaja na Nuru kubwa na kuiangazia juu yako, loo, daima nilivutiwa na hilo. Nawe ukaanza kuifuata hiyo Nuru, nao mlango ukafunguka mbele yako, ukakupeleka moja kwa moja barabarani. Ulidhani unaota." Ni wakati wa jinsi gani!

137 Hakutakuwa na mahali patulivu Mbinguni, wakati wote waliokombolewa watakapofika Huko, sivyo? Litakuwa ni jambo la kustaajabisha litakalotukia huko Juu, wakati wote waliokombolewa watakapoingia wakitembea taratibu.

138 Na huyu hapa akida huyu, nyumba ya Kornelio. Angalieni jinsi Mungu alivyolipanga! Sasa, Kornelio alikuwa ni mtu mcha Mungu. Aliomba daima, na kuwapa watu sadaka. Hufanyi chochote cha thamani pasipo Mungu kukiweka kwenye kumbukumbu yako. Hiyo ni kweli. Naye akaomba, na kuwapa watu sadaka. Naye alikuwa mtu mashuhuri.

139 Ndipo siku moja, alipokuwa katika maombi nyumbani, Malaika aliingia katika chumba alimokuwa. Mnaamini katika Malaika? Malaika aliingia chumbani alimokuwa, akasema, "Kornelio, amka uende Yafa. Na ukaulizie mtu mmoja jina lake Petro, akaaye katika nyumba ya mtu aitwaye Simoni. Naye atakwambia la kufanya." Amina.

140 Sasa, Petro, wakati huu, alikuwa akisafiri, kwa hiyo akaona njaa. Ilikuwa yapata saa sita. Kwa hiyo, anapanda juu ya paa la nyumba na kulala kidogo. Alikuwa anaenda kulala kidogo akiwa pale juu, akisubiri waandae chakula cha jioni.

141 Na kwa hiyo Kornelio akatuma mtu kule, ni askari na watu wawili watauwa, naye akawaleta huko chini kumtafuta Petro.

142 Na wakati, Mungu, kama anamtuma mtu kukuona, anafanya maandalizi kabla ya wakati kwa jambo hili kutokea.

143 Alifanya maandalizi hospitalini, kwa ajili ya mtoto huyu mchanga jana, aliyekuwa amelazwa pale mahututi, ambapo hawakujua kuna shida gani. Ndipo Roho Mtakatifu akanena chumbani; akafanya maandalizi hospitalini, kwa ajili ya uponyaji wa huyo mtoto kabla hata sijafika pale. Haleluya!

144 Huko Ufini, wakati mvulana huyo mdogo alipokuwa amelala pale barabarani, amekufa. Nao baba na mama yake, wakikimbia kutoka shambani, wakipiga mayowe, na kuminya mikono yao. Mungu alikuwa amefanya maandalizi ya kufufuka kwake awali, miaka miwili kabla ya wakati. Bwana asifiwe!

145 Basi, usiku wa leo, wakati tukiwa hapa katika kanisa hili, na kuteseka mambo haya tunayopitia, Mungu amepanga awali ufufuo wetu. Siku fulani tukufu, Yeye atakuja. Yote yamepangwa kimbele. Na wanaume na wanawake wanaowazia juu yake, wakati mwingine washairi huimba nyimbo hizi "Loo, kutakuwa na mkutano angani."

146 Yapata miaka kumi na mitano iliyopita, usiku wa leo, nilikuwa nimesimama kwenye jukwaa hili hapo, nikiwa na chati kubwa, nikifundisha.

147 Basi kulikuwa na maskini kundi dogo la Wapentekoste lililotoka Louisville. Na kamwe sikuwahi kuwaamini watu hao kucheza jinsi walivyocheza. Na kulikuwa na maskini msichana

mmoja aliyekuja hapa kucheza piano. Nao walikuwa wakitaka kucheza wimbo maalum, na kupiga ninii ndogo. . .kupiga ubao wa kuoshea kwa kastabuni. Na baadhi yao wakapiga kopo la bati. Nilikuwa mkosoaji wake sana, kwa hivyo nikawazia, "Itakuwaje?" Ndipo mwanamke mmoja akaja kucheza wimbo maalum. Akaanza kucheza. Mama huyo akaingilia kupiga ule ubao wa kuoshea. Ndipo msichana huyu mdogo mwenye nywele nyeupe akaruka kutoka hapa, sakafuni, na kuanza kucheza katika Roho.

148 Huku mimi, nikiwa nimeketi barazani pa wenye mizaha, nikasema, "Sasa, laiti ungeliangalia hilo!" Nami nilikuwa nikiliambia kanisa langu, hata wote walikuwa wanashangaa nitafanya nini kuhusu jambo hilo. Niliendelea kumtazama, nami nikawaza, "Angalia hiyo! Sasa, kama hilo si jambo fulani! Kufanya kanisa langu kilabu ya pombe!" Nami nilikuwa nimeketi pale, bila kujua bora zaidi. Sikuwa nikisema chochote, lakini moyoni mwangu nilikuwa nikiliwazia.

149 Kwa hiyo nikamtazama pale alipokuwa akicheza. Na muda si muda mwajua, nikasema, "Sasa hebu kidogo. Sijui kama mama huyo ana Maandiko yoyote kwa ajili yake?" Ndipo nikaanza kufikiria juu ya Maandiko. Nikasema, "Uchezaji dansi uliwahi kuruhusiwa wapi? Kwanza kabisa, katika Biblia." Hiyo ni kweli. Nami nikawazia, "Ni nini kiliwafanya wacheze dansi?"

150 Nikaona ya kwamba wana wa Israeli, walipovuka Bahari ya Shamu, Miriamu aliangalia nyuma akaona wale wasimamizi wote wamezama, akachukua tari na kuanza kucheza; na kupiga tari hii, na kukimbia ufukoni, akicheza. Nao binti za Israeli wakamfuata, wakicheza. Nikawazia, "Huo ni ushindi."

151 Nikamwona Daudi, huku mchumba wake ameketi kule nyuma ya feni hii, akijipepea, akimtazama rafiki yake mvulana mwenye sura ya kupendeza, Daudi amesimama huko nje. Na hili hapa sanduku linakuja, ambalo Ndugu Graham alizungumza habari zake muda mfupi uliopita, likipitia kilimani. Wakati Daudi alipoliona likija, alicheza akizunguka na kuzunguka na kuzunguka. "Mbona," akasema, "unaniaibisha!"

152 Akasema, "Ikiwa hupendi hiyo, tazama hii!" Naye akazunguka na kuzunguka na kuzunguka tena.

153 Mnajua nini? Mungu alitazama chini kutoka Mbinguni, akasema, "Daudi, wewe ni mtu anayeupendeza moyo Wangu Mwenyewe." Hiyo ni kweli.

154 Nami nikawazia, "Unajua, kuna jambo moja lililo shida yangu. Sijapata ushindi wa kutosha, labda." Nami nikaendelea kuketi pale, kisha nikaanza kuupigapiga mguu wangu wa Kimethodisti. Na muda si muda mwajua. . .Mungu, hakimu wangu! Mimi, kabla sijajua nilichokuwa nikifanya, nilikuwa nje sakafuni hapa, nikicheza huku na huko, pamoja na msichana huyo. Hiyo ni kweli.

155 Kisha nikasema, “Mungu, nitoe barazani pa wenye mizaha. Jalia niangalie jambo lolote kwa busara kabla sijatoa hukumu tena.” Amina. Mungu hufanya mambo ya kipekee.

156 Siamini katika upuuzi mwingi. Siamini katika upuuzi chungu nzima. Lakini ninaamini katika Neno halisi la Mungu, lililojazwa Roho Mtakatifu, linalohubiriwa kwa nguvu na madhihirisho. Amina. Kwa maana, Hicho ndicho kitu kilichoniokoa. Hicho ndicho kitu kilichonileta umbali huu. Hicho ndicho kitu kilichonisaidia hapo daktari aliposema nilikuwa nafa. Hicho ndicho kitu kilichoniokoa katika saa ya kufa kwangu. Hicho ndicho kitu kitakachonifufua. Na Hicho ndicho kitu nitakachokwenda nacho Mbinguni. Nikiwahi kufika Huko, itanibidi kwenda na Hicho; kwa sababu sijui kitu kingine ila Hicho, wala sitaki kujua kitu kingine ila Hicho. Hiyo ni kweli.

157 Nimjue Yesu, Naye amesulubishwa, hamna lingine. Kama amesulubishwa, basi inasulubisha mwili wangu pamoja na Wake, nami nimekufa kwa mambo ya ulimwengu. Kwa nini! Amina!

Mnajua, ninaanza kujisikia kubarikiwa. Ninaanza kujisikia hivyo.

158 Angalieni, hawa hapa. Jamani, ni wakati wa jinsi gani! Walikuwa na mkutano wa ajabu! Kornelio akasema, “Sasa shuka kule ukaulizie mtu anayeitwa Petro.” Naye akasema . . . Sijawahi kusikia habari zake hapo kabla.

159 Naye Petro huko juu, akawazia, “Bwana, nitalala kidogo kabla tu sijala chakula cha jioni. Nina njaa sana na ni mchovu.”

160 Basi alipokuwa amelala pale, akaingia katika njozi. Maandiko yanasema hivyo. Basi, ninaamini aliingia katika njozi, sivyo? Na alipofanya hivyo, aliona shuka likishuka, lote limejaa vitu vitambaavyo. Ndipo Sauti ikasema, “Amka, Petro. Chinja na ule.”

161 Akasema, “Hasha, Bwana. Mimi ni Myahudi. Hakuna kitu kichafu ama najisi ambacho kimewahi kuingia kinywani mwangu.”

162 Akasema, “Usiviite najisi nilivyovitakasa.” Kasema, “Amka wewe.” Kasema, “Kuna mtu anayekungojea, pale chini langoni. Basi endelea, usitilie shaka chochote. Mfuate.” Amina.

163 Sasa, Petro, na njia zake za utakatifu, mwajua. Kwa namna fulani alikuwa na sifa njema kwa watu, kwa hiyo ilimbidi aangalie anachokula. Alikuwa Myahudi. Alikuwa amelelewa, M—Mpresbiteri mkali, mwajua, ama kitu fulani, na ilimbidi aangalie alichokuwa akifanya kwa sababu ya mambo yake ya kanisa.

164 Basi Bwana akasema, “Wafuate hao Wamataifa, bila kuzingatia chochote kinachofanywa, au chochote kile. Panda huko juu.”

165 Naye alipopanda hadi nyumbani kwa Kornelio, mara, Kornelio akawakusanya watu wake wote hapo. Naye akamwambia jinsi alivyomwona Malaika. Akasema, “Sasa, Petro, ni—nimeagizia uitwe.”

166 Ndipo Petro aliposimama pale na kuanza kuhubiri, “Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia,” nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kutabiri, kunena kwa lugha, na kuwa na wakati wa ajabu. Akasema, “Je, tunaweza kukataza maji?” Sasa, hawa wamempokea Roho Mtakatifu kabla hawajabatizwa. Naye akaamuru wabatizwe kwa Jina la Bwana Yesu. Naye Petro akakaa nao siku kadha wa kadha.

167 Hilo ndilo Kanisa la kimitume, likitembea katika Roho, popote Mungu aliposema. Petro akaenda bila chakula chake cha jioni. Petro akashuka, kumfuata Bwana.

168 Basi kama Mungu angaliweza kumpata mwanaume na wanawake leo, katika maskani hii, popote pengine, ambao hawatajali kinachoendelea karibu nao, bali wajisalimishe kwa Bwana, kama kitengo cha mtu binafsi, Mungu atamwongoza mtu yuyo huyo leo, ambavyo Yeye aliongoza wakati huo. Anathibitisha ya kwamba yuko pamoja nasi. Tunachohitaji leo ni maisha ya unyenyekevu, ya kujitolea. Jitolee mwenyewe. Usijirudishe nyuma. Usifanye chochote ila uongozwe moja kwa moja na Roho Mtakatifu. Kile Roho asemacho ufanye, kifanye upesi. Usiseme, “Vema, nitasubiri nijue *hii* ni nini, na *hiyo* ni nini.” Kile Roho Mtakatifu anachosema ufanye, nenda ukakifanye!

169 Vipi kama nisingeenda Ufini wakati Roho Mtakatifu aliponiita kule? Vipi kama nisingeenda hospitalini jana, ambako mtoto huyo mchanga alikuwa amelala pale akifa; sikuenda?

170 Ni, “Kutii ni bora kuliko dhabihu.” Fanya yale Roho Mtakatifu anasema ufanye. Tunachohitaji usiku wa leo, ni kuachilia mawazo yetu yote madogo ya kale yanayobana, na kumwacha Roho Mtakatifu. . .Mnafundishwa hapa. Mnajua mema na mabaya.

171 Lakini unachohitaji usiku wa leo ni lundo kubwa la upendo wa Mungu limiminiwe moyoni mwako; tofauti zote ziondolewe mbali. Uzizike na mwaka wa kale, unapopita. Acha ziende. Hebu tuanze maisha mapya, mwanzo mpya. Huwezi. . .Ikiwa tayari umezaliwa katika Ufalme wa Mungu, tayari unaye Roho Mtakatifu ndani yako, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kujitenga na mambo haya ya ulimwengu ambayo yanakufinyilia chini. Kasema, “Na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ituzingayo kwa upesi; ili tupige mbio kwa saburi, maisha, yale

mashindano yaliyowekwa mbele yetu." Waebrania, mlango wa 12. Weka kando mizigo mizito!

172 Ungeweza kuwazia wale mamajusi wakija kumwona Yesu? Nitachukua mchezo mdogo tu wa kuigiza kwa dakika moja. Naweza kuona. . . Wanasema mamajusi watatu. Tutasema tu kulikuwa na watatu. Jim, John, na George, tungesema majina yao yalikuwa hayo. Nao wanakuja kumwona Yesu. Na ninaweza kuwaona wote wakijiandaa kwenda. Tutamchukua jamaa huyu Jim. Yeye ni mwanaume kweli kweli. Anakimbia na kumwambia mkewe, kasema, "Mke wangu, unajua nini? Niliiona ile nyota, kwa hivyo sina budi kwenda." Na kwa hiyo anaenda na kupakia, ili aende.

173 Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi. Wanajaribu kujifungia mizigo, wapate kuwa Mkristo. Kama kuna chochote unachohitaji, ni "kuondolewa mizigo," upate kuwa Mkristo. Una mambo mengi kupita kiasi yanayoning'inia sasa.

174 "Mama!" Kasema, "Sasa, mama, unajua, nisingeweza kwenda mbele isipokuwa nichukue meza yangu ya karata," kwa hiyo anaining'iniza hiyo juu ya ngamia. "Kwa sababu, mwajua, hao wavulana wengine hawangenifurahia mimi kwenda nao iwapo sikuja na meza yangu ya karata."

175 Mambo haya mengine yote madogo madogo ya kale ambayo yanakuweka. Nawe una kijisanduku cha ubinafsi, inakubidi kuning'iniza hicho, pia. Pia huna budi kuning'iniza umbeya kidogo, masengenyo kidogo, kidogo ya *haya, yale*, uyaning'inize juu ya ngamia.

176 Ndipo muda si muda mwajua, yeye anaruka juu, akimtagaa ngamia mzee, na kusema, "Hima! Twende!" Maskini huyo ngamia mkongwe anaenda kwa shida. Amepondwa chini kwa nguvu sana mpaka karibu ana miguu ya matege.

177 Na sikuzote unapiga teke na kulalamika kuhusu kanisa lako unalohudhuria, na labda umefungiwa mizigo sana hata haliwezi kukimbia. Hiyo ndiyo shida. Unahitaji kuondolewa mizigo, kuosha, kusafisha, uwe sawa. Amina. Nina shida gani? Angalieni. Hivyo ndivyo ilivyo.

178 Ninaweza kuwaona hao wengine wakienda, wakiendelea. Na muda si muda mwajua, alishuka na kuitazama nyota hiyo tena. Na kwa hiyo, jambo la kwanza, akaanza kutupa meza upande mmoja, na vifurushi upande mwingine.

Mke akasema, "Unaenda wapi, John?"

179 Kasema, "Ninaweka kando kila mzigo mzito unaonizinga kwa upesi. Kwamba, sina budi kupiga mbio hizi kwa subira. Kwa maana mlango ni mwembamba na njia imesonga, lakini watakaoipata ni wachache." Kuna nafasi tu kwako wewe na Yesu. Hakuna mtu mwingine anayeweza kupita. Amina.

180 Alisema. Naweza kumsikia akisema, “Vema, angalia, unasahau dira yako.”

“Sihitaji dira yoyote.”

181 “Unasahau digrii yako ya seminari. Unasahau huduma zako za shahada ya mwisho na mambo haya mengine yote ambayo unashikilia.”

Akasema, “Sikiliza. Sihitaji dira yoyote.”

“Utaendaje basi?”

182 Akaelekeza kwa nyota, akasema, “Ninaenda kwa njia iliyoandaliwa na Mungu. Mungu alinipa nyota ya kufuata, ambayo itanipeleka kwa Kristo.”

183 Na usiku gani? Hatuhitaji masomo yoyote makubwa, marefu, na haya yote. Tunataka kwenda kwa njia iliyoandaliwa na Mungu. Na njia ya Mungu iliyoandaliwa na Mungu ya siku hizi ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuongozwa na Roho Mtakatifu, ni wana wa Mungu. Hiyo itakufikisha kwenye kikomo chako. Weka kando mizigo mizito. Weka kando kila kitu kingine. Hebu turudi kwenye siku za mitume. Msingi wetu ni wa hakika.

184 Mungu ametuandalia huo, kwa ishara, na maajabu, na picha, na chochote kile. Amethibitisha kwamba Yuko pamoja nasi.

185 Na ulimwenguni kote, Injili hii tukufu yenye nguvu iliwaleta watu milioni moja na laki tano katika Ufalme wa Mungu, mwaka jana. Kanisa la Kipentekoste lilichukua nafasi ya kila kanisa lililokuwako ulimwenguni mwaka jana, katika uongofu, milioni moja na laki tano waliorekodiwa. Haleluya! Kuna nini? Ndicho kitu chenye nguvu kuliko vyote kilichopo duniani leo. Lakini Ibilisi ameingia kati yao na kuwatenganisha katika kundi *hili* dogo, na kundi *lile* dogo, na kundi *hili* dogo, kuwafanya wabishane wao kwa wao.

186 Kama kamwe wangesahau ubinafsi wao na tofauti zao, na kuunganisha mikono yao pamoja, mioyo yao pamoja, kama mmoja, ule Utawala wa Miaka Elfu ungeingia. Hilo ndilo tunalohitaji usiku wa leo, ewe rafiki, na tujumuike pamoja. Hilo ndilo Maskani ya Branham inapaswa kufanya. Hilo ndilo makanisa yote yanapaswa kufanya, ni kukusanyika pamoja kama ushirika mmoja, kama mtu mmoja, katika Kristo Yesu, mtoto mchanga aliyezaliwa upya, na kutembea njia hii nyembamba, iliyonyooka, “Tukimtazama mwanzilishi na mwenye kutimiza imani yetu, Yesu Kristo.”

187 Angalieni hapa. Si kuitetea maskani yetu na Mafundisho yake, na kadhalika, lakini ninasema hivi, marafiki zangu wapendwa. Hebu tafuta ulimwenguni popote utakapo, na tunasema hivi kwa majivuno, sio kujivuna kwa chochote ila Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Lakini angalia yale Mungu Mwenyezi amefanya kwa ajili ya kanisa hili dogo. Geuka na uangalie, ukitaka. Moja kwa moja kutoka kwenye kanisa

hili hapa, ulianzishwa uamsho huu mkuu ambao umeenea ulimwenguni kote. Na hiyo ni kweli. Lichunguze tena, uone kama sivyo. Mungu yu pamoja nasi. Katika upendo Wake na rehema, angalieni jinsi anavyotuponya tunapokuwa wagonjwa. Angalieni wagonjwa wa kansa, na vipofu, viziwi na mabubu, na wowote wale anaowaponya katikati yetu, kila mahali. Halafu, alikuwa na upendo wa kutosha kushuka kwa ajili ya thibitisho la kisayansi, kuweka kibali Chake juu ya hili kanisa, akapigwa picha Yake pamoja nasi. Amina.

188 Ambapo, wakosoaji, itawabidi kufunga kinywa chao na kurudi nyuma, na kusema, "Siwezi kusema lolote kuhusu Hiyo." Amina.

189 Nina furaha sana usiku wa leo, kwamba mimi ni mmoja wao! Nina furaha sana kuwa Mkristo. Nina furaha sana kwamba ninaishi hapa kati ya watu wanaoamini katika hatua hii kuu. Ambao. . . Natarajia kuwe na tofauti ndogondogo. Sisi ni binadamu. Lakini, kimsingi, sisi ni mmoja. Kweli. Sisi ni mmoja. Pamoja twasimama, kama kitengo kimoja katika Yesu Kristo. Mungu ametubariki na kutupa mambo haya yote ya ajabu.

190 Hebu wazieni tu, jinsi ni—nisingekuwa hapa mimi mwenyewe, usiku wa leo, kama isingalikuwa kwa ajili ya Bwana, wakati madaktari walio bora sana walisema nisingepona. Lakini Daktari Mkuu akashuka na kusema, "Yote yako mikononi Mwangu, na utapona." Nikamwamini.

191 Dada Weaver anayeketi hapo yukoje? Kama gofu la mtu katika kile kiti cha magurudumu, walipomsukuma hapa juu ili abatizwe kwa Jina la Yesu Kristo; daktari alimpa hadi asubuhi, kuishi, huku akiliwa na kansa, yapata miaka saba ama minane iliyopita. Huyu hapa usiku wa leo pamoja nasi.

192 Ni wangapi zaidi ambao ningeweza kuwaita, ambao wameingia na kutoka kwenye milango hii hapa, ambao wameingia hapa, viwete, na wanaoteseka, na wagonjwa, na vilema, na wasiojiweza, vipofu, na chochote kile, wameponywa. Katika mlango huu mdogo tu hapa, kama shahidi wa kufufuka kwake Bwana Yesu Kristo!

193 Tunapaswa kuwa nini? Maskani hii ya Branham inapaswa kuwa nini? Inapaswa kuwa mnara wa taa ambao umewekwa katika mojawapo ya maeneo yenye giza sana ulimwenguni, Jeffersonville. Kama kuliwahi kuwa na mahali palipohitaji Injili, ni Jeffersonville. Hiyo ni kweli.

"Lakini je, kitu chochote chema kinaweza kutoka Nazareti?"

Kasema, "Njoo uone." Hiyo ni kweli.

194 Maeneo ya giza! Hatuhitaji taa mchana. Tunazihitaji wakati kuna giza. Hapo ndipo Mungu anapotuma Nuru, ni mahali penye giza. Ni vigumu sana . . . Rahisi kwenda mahali ambapo kila kitu

kinaenda vizuri. Lakini mahali penye ugumu, sehemu zenye giza, mahali pabaya!

> Je, yanibidi kupelekwa nyumbani Mbinguni
> Kwenye kitanda cha maua cha urahisi,
> Wakati wengine walipigana wapate kushinda tuzo,
> Na kuabiri katika bahari zilizojaa damu?

195 Papa hapa ambapo watu wanabishania tofauti ndogondogo, na mambo kama hayo; makafiri mia moja na arobaini elfu hufa kila siku, na kwenda kukutana na Yesu, au kwenda kukutana na Mungu mwenye haki na mwaminifu, bila kujua chochote kumhusu. Laki moja na arobaini elfu hufa kila siku, idadi ya vifo vya makafiri ambao hawakuwahi kusikia Jina la Yesu Kristo, wanakufa kila siku. Nasi tunabishana kama sisi ni Presbiteri ama Mmethodisti, ama sivyo. Ni fedheha jinsi gani! Ni aibu jinsi gani!

196 Tunachohitaji ni ono. Sio kuangalia hapa chini mwishoni mwa pua yako. Angalia huko nje mwishoni mwa safari. Kama ninawazia kuhusu leo, *hili*, *lile*, ama *linginelo*, nitaiishia siku hii. Lakini ninauishia Umilele, kwa ajili ya kitu fulani huko ng'ambo, kitu ambacho Mungu amekiweka, nami sina budi kwenda kukutana nacho siku moja.

197 Nimechukua muda mwingi mno; dakika kumi. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .kwa neema ya Mungu na msaada wa Mungu.

198 Kumekuwa na miaka miwili ambayo nimemwomba jambo fulani, tena na tena. Nilimwomba miaka kumi na mitano, jambo fulani, na hatimaye akanipa. Nami nitakuwa nikibisha mlangoni Pake, kama nitaishi mwaka ujao, kama hatanipa mwaka huu, mnaona, kwa ajili ya jambo hili ambalo nimeombea. Ni kwa ajili ya Utukufu Wake, jambo ambalo ningeweza kumfanyia Yeye kule. Ataniruhusia tu jambo hili, ndipo ninaweza kwenda huko nje na kuwaleta watu Kwake, wengi kidogo, niwe na nguvu zaidi kidogo njiani. Nami naomba ya kwamba atafanya hivyo. Hayo ndiyo maombi yangu Kwake.

199 Na ushuhuda wangu kwenu, ya kwamba, kama mtaniombea tu na kunishikilia mbele Zake, katika maombi, basi naweza kuendelea. Ninawezaje kufanya jambo moja, haidhuru nini kingetukia, kama sikuwa na mtu wa kuniamini? Ninyi ni sehemu yake tu kadiri nilivyo mimi, au mtu mwingine yeyote alivyo. Ninyi ni sehemu kubwa yake. Haidhuru tungefanya nini, kama tungehubiri, yale tungesema; ikiwa hakuna mtu wa kuliamini, basi hakuna kinachoweza kufanywa. Hiyo ni kweli. Yote yameshindikana, hakuna kinachoweza kufanywa, isipokuwa tuje pamoja na kuaminiana. Nikuamini nawe uniamini. Na, pamoja, tunamwamini Mungu, nasi tunaamini ya kwamba Roho Wake atatuongoza.

200 Sasa, Ndugu Funk, unakuja? Unamshika mtoto sasa; huo ndio udhuru wako. Ndugu Wood, nadhani wewe ndiye unayefuata basi. [Ndugu Wood anasema, "Ndugu Jackson."—Mh.] Vema, naye amemchukua Ndugu Jackson. Kwa hiyo nadhani Ndugu Jackson ndiye atakayefuata. Bwana ambariki Ndugu yetu Jackson, anayefuata.

201 Bwana awabariki. Je, mna—mnampenda Bwana? Nataka kuona mikono yenu. Je, mnampenda Bwana? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

202 Dada Gertie, njoo hapa kwa dakika moja tu. Nataka uimbe mmoja pamoja nami. Wengine wote wanaimba. Nitajaribu. Nimepwelewa na sauti kabisa, kwa sababu nina homa kali, nami. . . kitu fulani, kichwa changu, lakini nataka unisaidie kuimba wimbo huu mzuri wa kale. Na unipe sauti ya. . . kitu fulani. Sijui ni nini. Lakini, sijui ni nini. Nipe tu aina fulani ya sauti, kwa sababu ninataka kuimba, *Kudondoka Damu*, pamoja nanyi nyote. Kwa maana, Injili hii ninayohubiri, inadondoka damu. Je, hamwamini? Vema, kila mtu, pamoja sasa.

> Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa Roho Mtakatifu,
> Alikuwa Yohana Mbatizaji, lakini alikufa kama mwanamume;
> Ndipo akaja Bwana Yesu, wakamsulubisha,
> Yeye alihubiri ya kwamba Roho angewaokoa watu kutoka dhambini.
>
> Inaendelea kudondoka damu, naam, inadondoka damu,
> Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
> Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,
> Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu.
>
> Lakini basi wakampiga kwa mawe Stefano, alihubiri dhidi ya dhambi,
> Akawafanya wakasirike sana, wakakiponda kichwa chake;
> Lakini alikufa katika Roho, akakata roho,
> Ndipo akaenda kuungana na wengine, jeshi hilo linalotoa uzima.
>
> Inaendelea kudondoka damu, naam, inadondoka damu,
> Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
> Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,
> Injili hii ya Roho Mtakatifu. . .
>
> Loo, kuna Petro na Paulo, na Yohana mtauwa,
> Waliyatoa maisha yao kusudi Injili hii ipate kuangaza;

Walichanganya damu yao, kama manabii wa kale
Kusudi Neno la kweli la Mungu lipate kuhubiriwa kwa uaminifu.

Inaendelea kudondoka damu, naam, inadondoka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inaendelea kudondoka damu.

Sikilizeni hii sasa:

Kuna roho chini ya madhabahu zinazolia, “Hata lini?”
Bwana apate kuwaadhibu wale waliotenda maovu;
Lakini kutakuweko na wengine watakaotoa damu ya uhai wao,
Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na mafuriko Yake yaliyo mekundu sana.

Tusimame sasa.

Inadondoka damu, naam, inadondoka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

203 Je, huna furaha kuwa wewe ni mmoja wao? Injili ya aina gani? Injili ile ile waliyopewa, ishara zile zile, maajabu yale yale yakifuata, Nguzo ile ile ya Moto, Bwana Yesu yeye yule, uponyaji ule ule wa wagonjwa, nguvu zile zile za Roho, kila kitu kikiendelea moja kwa moja. Mateso yale yale yanakuja.

Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

Sote kwa pamoja sasa.

Inadondoka . . .

204 Geuka na kupeana mikono na mtu, na kusema, “Bwana asifiwe!”

. . . dondoka damu,

205 Haleluya! Si wewe ni Ndugu . . .?. . . Bwana asifiwe! . . .?. . . Amina.

. . . inadondoka damu,
Loo, damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Kwani alinipenda kwanza.

Hebu tuimbe kwa sauti kuu zaidi sasa. Inueni mikono yenu.

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Kwani alinipenda kwanza.

206 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru usiku wa leo kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya Nguvu Zake, kwa ajili ya upendo Wake. Na kujua, ya kwamba, katika siku hii kuu, adhimu tunayoishi, manabii wa kale walipoiona siku hii, walitoa amri juu yake, wakisema ambavyo "watu wangekuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake." Aliposema, "Kutakuwa na watu wenye kudhihaki katika siku za mwisho, nao wangefanya mizaha, na dhihaka." Nasi tunaishi ndani yake, Baba.

207 "Siku hiyo, magari yangevuma katika njia kuu. Yangeenda mbio kama umeme. Yangeonekana kama mienge." Haya yote, unabii mkuu, unaotimia!

208 Yesu aliposema, "Mawimbi ya maji yangeingia ufukoni, huku na huku kwenye kingo za bahari. Na wakati ishara kuu na maajabu yangetokea kwenye mbingu juu, kama vile visahani virukavyo na kadhalika. Kwa sababu ya ishara hizi, ingesababisha ulimwengu kuogopa na kutetemeka. Ingesababisha matetemeko ya ardhi mahali mahali, na kila namna ya mambo; na fadhaa ya wakati, na dhiki kati ya mataifa."

209 Naye akasema, "Siku hiyo, kwamba Israeli ingesitawi." Haleluya! Hiyo nyota ya kale ya pembe sita ya Daudi inapepea juu ya Yerusalemu, usiku wa leo, kwa mara ya kwanza kwa miaka elfu mbili mia tano. Mataifa yanavunjika. Mtini ukichanua majani yake!

210 Miti hiyo mingine yote inatoa chipukizi zake. Waovu wanachipusha. Urumi unachipusha. Ukomunisti unachipusha.

211 Nalo Kanisa Lako linachipusha. Msimu wa kuchipua unakuja. Ee Bwana mkuu wa Uzima, inuka na uponyaji katika mbawa Zako, Bwana. Na uwape watumishi Wako nguvu na ishara zote, ili kuunyoosha mkono wa Mtoto Wako Mtakatifu Yesu, kufanya miujiza na kufanya ishara, na kuihubiri Injili hata miisho ya dunia. Tujalie, Bwana.

212 Libariki kanisa hili dogo. Mbariki mchungaji wake, Bwana, ndugu yetu mpendwa. Wabariki wote wanaohusishwa hapa pamoja nasi. Wote wanaoliitia Jina Lako, kila mahali duniani kote. Tusaidie, mwaka huu ujao, Bwana, tusaidie kuwa bora zaidi kwa huduma Yako. Ondoa magonjwa kati yetu. Na ututie

mafuta kwa Roho Mtakatifu. Weka wivu, weka ugomvi, weka kijicho, ondolea kila kitu kilicho kiovu, mbali nasi. Na jalia isemwe kwetu, kwamba sisi ni watoto Wako, "Mji unaokaa juu ya mlima, ambao hauwezi kufichwa." Tujalie, Baba.

213 Utubariki, na utusamehe yaliyopita. Na jalia tuseme, kama Paulo, "Tukisahau mambo ya kale, tunapiga mbio kuifikia mede ya mwito mkuu katika Kristo."

214 Bwana Mungu, nitume popote upendapo. Niko tayari kwenda, fanya upendavyo wakati wowote.

215 Tusamehe, nasema, tena. Na ulitakase kanisa hili kwa heshima na utukufu wa Jina Lako, na watu waliomo. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

216 Mwaweza kuketi sasa. Bwana awabariki.

Loo, vema, kutakuwa na mkutano hewani,
Kwa utamu, kwa utamu hivi karibuni;
Nitakutana nawe, tukutane Huko
Katika makazi hayo ng'ambo ya anga;
Kuimba kuzuri sana utasikia, hakujapata kusikiwa kwa sikio la mwanadamu,
Itakuwa adhimu, ninatangaza!
Kwa kuwa Mwana wa Mungu Mwenyewe, atakuwa Ndiye anayeongoza
Katika mkutano huo angani.

Loo, kutakuwa na mkutano hewani,
Kwa utamu, utamu hivi karibuni;
Ninakwenda kukutana nawe, kukutana nawe Huko
Katika Makazi hayo ng'ambo ya anga;
Kuimba kuzuri sana utasikia, hakujawahi kusikiwa na sikio la mwanadamu,
Itakuwa adhimu, ninatangaza!
Kwa kuwa Mwana wa Mungu Mwenyewe, atakuwa Ndiye anayeongoza
Katika mkutano huo hewani.

Mmesikia habari za maskini Musa kwenye kichaka,
Mmesikia habari za shupavu Daudi na lile kombeo;
Mmesikia hadithi ikisimuliwa ya Yusufu mwota ndoto,
Na ya Danieli na simba mnaimba mara nyingi.
Loo, kuna wengine wengi, wengi katika Biblia,
Na ninatamani kukutana nao wote, natangaza!
Hivi karibuni Bwana atatujalia kukutana nao
Katika mkutano huo hewani.

Kutakuwa na mkutano hewani,
Kwa utamu, kwa utamu hivi karibuni;

Tutakutana nawe, tukusalimie Huko
Katika Makazi hayo ng'ambo ya anga;
Kuimba kuzuri sana utasikia, hakujawahi kusikiwa na sikio la mwanadamu,
Itakuwa adhimu, natangaza!
Wakati Mwana Mwenyewe wa Mungu atakuwa Ndiye anayeongoza
Katika mkutano huo hewani.

217 Je, hamuupendi? Jamani! Kuna Mmoja ninayetaka kukutana Naye, zaidi ya wote, huyo ni Yesu. Nawe je? Inakufanya tu ujisikie kufurahishwa sana, kusafishwa sana, safi sana. Hivi hamjisikii hivyo tu? Ni kama kwamba mlisuguliwa tu kabisa! Mpendeni Yeye tu!

. . . mkutano angani,
Kwa utamu, kwa utamu hivi karibuni;
Ninakwenda kukutana nawe, na kukusalimia Kule,
Katika Makazi hayo ng'ambo . . .
. . . utasikia, hakujawahi kusikiwa na sikio la mwanadamu,
itakuwa adhimu, natangaza!
Na Mwana Mwenyewe wa Mungu atakuwa Ndiye anayeongoza
Katika mkutano huo hewani.

Je, humuupendi? Loo, jamani!

Mmesikia habari za maskini Musa kwenye kile kichaka,
Na mmesikia habari za shupavu Daudi na kombeo lake;
Mmesikia hadithi ikisimuliwa ya Yusufu mwota ndoto,
Na za Danieli na simba mnaimba mara nyingi.
Lo, kuna wengine wengi, wengi katika Biblia,
Nami ninatamani kukutana nao wote, natangaza!
Hivi karibuni Bwana atatujalia kukutana nao
Katika mkutano ule hewani.

Na, loo, vema, kutakuwa na mkutano angani,
. . . tamu, tamu hivi karibuni;
. . . nitakutana nawe, nikusalimu Kule
Katika Makazi hayo ng'ambo ya anga;
Kuimba kuzuri kulikopata kusikiwa, kusikiwa na sikio la mwanadamu,
Itakuwa adhimu, natangaza!
Na Mwana wa Mungu Mwenyewe atakuwa Ndiye anayeongoza
Katika mkutano huo hewani.

218 Jamani! Nataka tu kuwa Huko. Nawe je? Ni wangapi wanasema, “Kwa neema ya Mungu nataka kuwa huko.” Kwa neema Yako, Bwana! Bwana asifiwe.

Vema, Ndugu Neville.

Heri za mwaka mpya kwenu nyote. Mungu awabariki!

54-1231 Uzima Wa Milele Na Jinsi Ya Kuupokea
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org